# LEGAL AND HUMAN RIGHTS CENTRE

Justice Lugakingira House, Kijitonyama, P. O. Box 75254, Dar es Salaam, Tanzania
Telephone: 2773048, 2773038, Fax: 2773037, E-mail: lhrc@humanrights.or.tz
Website www.humanrights.or.tz


## TAARIFA KWA UMMA

## UAMUZI WA MAHAKAMA YA AFRIKA YA HAKI ZA BINADAMU NA WATU (ACHPR) WA KESI ZA UCHAGUZI NA DEMOKRASIA NCHINI TANZANIA

Leo tarehe 06 Machi jijini Arusha, Tanzania, Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu imetoa uamuzi wa kesi za uchaguzi na demokrasia katika Kikao cha 80 cha Mahakama hiyo. Kesi hizo ni kama ifuatavyo;

1) *Kesi yenye maombi namba 040/2020 ya Abdul Omary Nondo dhidi Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Kesi yenye maombi namba 043/2020 ya Deusdedit Valentine Rweyemamu na Paul Revacatus Kaunda dhidi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.*
2) *Kesi yenye maombi namba 046/2020 ya Ado Shaibu na wenzake dhidi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.*
3) *Kesi yenye maombi namba 041/2020 ya Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) na Leberatus Mwangómbe dhidi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania*

**Kesi yenye maombi namba 040/2020 ya Abdul Omary Nondo dhidi Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Kesi yenye maombi namba 043/2020 ya Deusdedit Valentine Rweyemamu na Paul Revacatus Kaunda dhidi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.**

Mahakama ya Afrika, imetoa uamuzi kuwa *Ibara ya 74(12) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977* na *Ibara ya 119(13) ya Katiba ya Zanzibar, 1984 inakiuka Ibara ya 3(2) na 7(1)(a) ya Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu (African Charter*), kwa kuweka zuio kwa Mahakama yoyote kuwa na mamlaka ya kuchunguza jambo lolote lilitotendwa na Tume za Uchaguzi (NEC, ZEC)katika kutekeleza madaraka yake.

*Sambamba na uamuzi huo, Mahakama imetoa amri zifuatazo kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;*



**Board of Directors:**
**Justice (Ret'd) Dr. Fauz A. Twaib- Chairperson, Ms. Josephine A. Zimba- Vice Chairperson, Dr. Anna Henga (Adv.) Secretary, Ms. Anabahati Mlay- Member, Ms. Hellen Kilontsi – Member, Dr. Ringo Tenga – Member, Dr. Ally Laay - Member, Dr. Abdullah H. Mohammed - Member, Ms. Lutgard Kokulinda Kagaruki - Member**

1. Kufanya marekebisho ya Katiba kwa kufuta *Ibara 74(12) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977 pamoja na Ibara 119(13) ya Katiba ya Zanzibar, 1984.*
2. Kuchapisha hukumu ya mahakama kuhusu kesi hiyo ndani ya kipindi cha miezi **mitatu (3)** kwa kuweka nakala ya Kiswahili na Kiingereza kwenye tovuti ya Mahakama ya Tanzania na Wizara ya Katiba na Sheria nakala hizo zipatikane kwenye tovuti hizo angalau katika kipindi cha mwaka mmoja.
3. Kutoa taarifa ya utekelezaji wa maamuzi hayo kwa Mahakama ya Afrika ndani ya **miezi kumi na mbili (12)** na kuendelea kufanya hivyo kila baada ya **miezi sita (6)** hadi Mahakama itakaporidhika na utekelezaji wa hukumu hiyo.

**Kesi yenye maombi namba 046/2020 ya Ado Shaibu na wenzake dhidi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.**

Mahakama ya Afrika, imetoa uamuzi kuwa *Ibara ya 41 (7) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977* kwa kuwa inakiuka *Ibara ya 1 na 7(1) ya Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu (African Charter),* kwa kuweka kinga na zuio la mahakama yoyote kuwa na mamlaka ya kusikiliza shauri la pingamizi dhidi ya mgombea aliyetangazwa na Tume ya Uchaguzi kuwa mshindi wa nafasi ya Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

1. Kufanya marekebisho ya *Katiba kwa kufuta Ibara 41(7) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977* ndani ya mwaka mmoja.
2. Kuchapisha hukumu ya mahakama kuhusu kesi hiyo ndani ya kipindi cha **miezi sita (6)** kwa kuweka nakala ya Kiswahili na Kiingereza kwenye tovuti ya Mahakama ya Tanzania na Wizara ya Katiba na Sheria nakala hizo zipatikane kwenye tovuti hizo angalau katika kipindi cha mwaka mmoja.
3. Kutoa taarifa ya utekelezaji wa maamuzi hayo kwa Mahakama ya Afrika ndani ya **miezi sita (6)** na kuendelea kufanya hivyo kila baada ya **miezi sita (6**) hadi Mahakama itakaporidhika na utekelezaji wa hukumu hiyo.

***Kesi yenye maombi namba 041/2020 ya Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) dhidi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania***

Kesi hii inahusu zuio la lilipo katika *Ibara ya 5(2)(c) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977* na iliyokuwa Sheria ya Uchaguzi ya 1985, zuio la wafungwa na watu walionje ya nchi (*diaspora)* kutoshiriki katika uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani. Upande wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania uliweka pingamizi la kuwa Mahakama ya Afrika haina mamlaka ya kusikiliza



**Board of Directors:**
**Justice (Ret'd) Dr. Fauz A. Twaib- Chairperson, Ms. Josephine A. Zimba- Vice Chairperson, Dr. Anna Henga (Adv.) Secretary, Ms. Anabahati Mlay- Member, Ms. Hellen Kilontsi – Member, Dr. Ringo Tenga – Member, Dr. Ally Laay - Member, Dr. Abdullah H. Mohammed - Member, Ms. Lutgard Kokulinda Kagaruki - Member**

kesi hiyo, pia kesi hiyo ilipaswa kuanzia katika Mahakama za Tanzania kabla ya kwenda kwa Mahakama hiyo kwa kuzingatia Sheria ya Utekelezaji wa Wajibu na Haki za Misingi (BRADEA).

Hata hivyo, Mahakama imetoa maamuzi kuwa, ina mamlaka ya kusikiliza kesi hiyo. Pia, imekataa pingamizi la ulazima wa mlalamikaji kuzingatia masharti ya Sheria ya BRADEA badala yake imekubali kuwa mlalamikaji anatakiwa kutafuta nafuu za kisheria katika mahakama za ndani kwa kuwa shauri hilo linagusa Katiba ya nchi husika. Kwa upande mwingine, mahakama imehifadhi mamlaka yake ya kuendelea na shauri la msingi la kesi hiyo siku zijazo.

**Imetolewa leo Machi 9, 2026 na:**

**Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC)**

**Dkt. Anna Henga**
**Mkurugenzi Mtendaji**

https://everify.humanrights.or.tz/verify?code=Pdx3Wp



**Board of Directors:**
Justice (Ret'd) Dr. Fauz A. Twaib- Chairperson, Ms. Josephine A. Zimba- Vice Chairperson, Dr. Anna Henga (Adv.) Secretary, Ms. Anabahati Mlay- Member, Ms. Hellen Kilontsi – Member, Dr. Ringo Tenga – Member, Dr. Ally Laay - Member, Dr. Abdullah H. Mohammed - Member, Ms. Lutgard Kokulinda Kagaruki - Member